

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**KIKAO CHA SITA**

**13 APRILI, 2023**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

### MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**KIKAO CHA SITA – TAREHE 13 APRILI, 2023**

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**III. MASWALI:**

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**68. MHESHIMIWA NASHON WILLIAM  
BIDYANGUZE (KIGOMA KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itaanza kujenga Majengo katika Kituo cha Afya Nguruka kilichopandishwa hadhi kuwa Hospitali.

**69. MHESHIMIWA NEEMA GERALD  
MWANDABILA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga barabara ya mchepuko kutoka Mpemba kupitia Chapwa Mwakakati katika Mji wa Tunduma kwa kiwango cha lami.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**70. MHESHIMIWA ISSA ALLY MCHUNGAHELA  
(LULINDI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, Serikali haioni haja ya kuwa na Chuo cha VETA katika kila Jimbo ili kuwakomboa Vijana na tatizo la ajira.

**WIZARA YA NISHATI:**

**71. MHESHIMIWA ALLY MOHAMED KASSINGE  
(KILWA KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha utekelezaji wa Sera ya kupeleka Umeme Vijijini kupitia Mpango wa REA III Mzunguko wa Pili.

## **WIZARA YA AFYA:**

### **72. MHESHIMIWA JESCA JONATHANI MSAMBATAVANGU (IRINGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, lini Serikali itapitia upya masharti ya fomu za bima ya afya ili kuondoa upotevu wa fedha za Vituo vya Afya kwa kushindwa kujaza fomu hizo.

## **WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

### **73. MHESHIMIWA TASKA RESTITUTA MBOGO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, kuna mkakati gani wa kuruhusu Mabasi ya Abiria yanayopita Wilayani Sikonge kuendelea na safari badala ya kuyalazimisha kulala.

## **WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

### **74. MHESHIMIWA MRISHO MASHAKA GAMBO (ARUSHA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini Wananchi wa Kata ya Moshono katika barabara ya mzunguko ya Kona ya Kiserian watalipwa fidia.

**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA  
TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**75. MHESHIMIWA JUDITH SALVIO KAPINGA  
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari,  
Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, ni upi mkakati wa kurahisisha matumizi ya  
Kibenki kwa njia ya Simu kwa kutumia Bando za  
Simu badala ya salio la Simu la kawaida.

**WIZARA YA KILIMO:**

**76. MHESHIMIWA ABEID IGHONDO RAMADHANI  
(SINGIDA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Miradi ya Umwagiliaji katika Vijiji vya  
Msange na Mnghamo – Singida Kaskazini  
itakamilika.

**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

**77. MHESHIMIWA BONIPHACE MWITA GETERE  
(BUNDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na  
Mipango:-

Je, kuna mkakati gani wa kupata mkopo wa  
fedha wa muda mrefu kwa masharti nafuu ili  
kulipa madeni sumbufu ya Awamu zote 6.

## **WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

### **78. MHESHIMIWA YAHAYA OMARY MASSARE (MANYONI MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, kuna mpango gani wa kupanda Hifadhini mazao yanayofuatwa na Wanyama waharibifu toka Hifadhi za Rungwa, Muhesi na Kizigo.

## **WIZARA YA MAJI:**

### **79. MHESHIMIWA REUBEN NHAMANILO KWAGILWA (HANDENI MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Bwawa la Mandela Kwenjugo na Kamkole Mabanda.

## **IV. HOJA ZA SERIKALI:**

### **WAZIRI MKUU:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

*(Majadiliano yanaendelea)*

**DODOMA  
13 APRILI, 2023**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**